PUBLIC PROCUREMENT APPEALS AUTHORITY
Efficient and Fair Appeals Dispensation
PPAA
MAMLAKA YA RUFANI YA ZABUNI ZA UMMA

"KAA TAYARI"
Complaints & Appeals

PPAA

Toleo Na: 09 Aprili - Juni 2026

# BULLETIN

"UTATUZI WA MIGOGORO KWA HAKI NA WAKATI"



*Katibu Mtendaji - PPAA*
*Bw. James Sando*

## Vijana, makundi maalumu Dodoma, Ruvuma wanolewa kuhusu haki, fursa ununuzi wa umma

**MPENDWA msomaji wa Jarida la "PPAA Bulletin" karibu tena ujisomee Toleo la Tisa (09) la Jarida la Mtandaoni kutoka Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA). Jarida hili ni moja kati ya njia inazozitumia PPAA katika mawasiliano yake ya kimkakati ya kuwahabarisha wadau wa ununuzi wa umma na umma kwa ujumla kuhusu shughuli mbalimbali zilizotekelezwa kwa kipindi cha miezi mitatu.**

Ninayo furaha kukuletea Toleo la Tisa la PPAA Bulletin kwa kipindi kingine tena cha miezi mitatu (Aprili – Juni, 2026), kwa lengo la kukuhabarisha shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi hicho.

Mbali na kutekeleza jukumu lake la msingi la kushughulikia malalamiko na rufaa zilizowasilishwa mbele yake kwa kipindi tajwa, PPAA imefanikiwa kutoa elimu kwa vijana, wafanyabiashara, wakandarasi, watoa huduma na wadau wa ununuzi wa umma pamoja na makundi maalumu wa mikoa ya Dodoma na Ruvuma na kuwasihi kutumia kikamilifu fursa zinazopatikana katika zabuni za umma.

Kadhalika, PPAA imeshiriki katika uzinduzi rasmi wa Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Mnyororo wa Ugavi ya Mwaka 2025, ambapo sera hiyo itazisaidia mamlaka, taasisi na wadau wote kuzingatia misingi ya utawala bora, uwazi na utawala wa sheria.

Katika toleo hili, tumekuandalia habari zinazohusu utekelezaji wa majukumu ya PPAA katika kufikia malengo iliyokusudia kwa kipindi tajwa ikiwa ni pamoja na kushiriki maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyoandaliwa na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ikiwa ni sehemu ya jitihada za serikali kuimarisha uelewa wa wananchi kuhusu fursa na haki katika michakato ya ununuzi wa umma.

Karibu usome jarida hili ili ufahamu kwa undani PPAA na shughuli ilizozitekeleza katika kipindi cha miezi mitatu (Aprili – Juni, 2026) na kuendeleza ushirikiano imara katika utoaji rufaa kwa ufanisi, wakati na kwa haki kwenye sekta ya ununuzi wa umma.

***#Kazi na Utu, Tunasonga Mbele.***
***Karibu Sana***

# Moduli ya Rufaa kuboresha mnyororo wa ugavi



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tan-zania, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba (Mb), (kulia), akiwa na Waziri wa Fedha, Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar (Mb), na viongozi wengine wakisikiliza maelezo kutoka kwa Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando (kushoto), kuhusu mchango wa PPAA katika mnyororo wa ugavi, wakati Mhe. Waziri Mkuu alipotembelea banda la maonesho la PPAA katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete, Aprili, 2026 jijini Dodoma kabla ya kuzindua rasmi Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Mnyororo wa Ugavi ya Mwaka 2025.*

**MAMLAKA ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imesema ujenzi wa moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa katika mfumo wa NeST utachangia kuongeza uwajibikaji, uwazi na ufanisi kwenye mnyororo wa ugavi.**

Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando amebainisha hayo wakati wa uzinduzi rasmi wa Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Mnyororo wa Ugavi ya Mwaka 2025 na kuongeza kuwa moduli hiyo imewaunganisha wazabuni wote na taasisi nunuzi nchini ili kuongeza uwajibikaji katika utatuzi wa migogoro inayotokana na michakato ya ununuzi wa umma.

"PPAA ni moja kati ya taasisi zinazosimamia ununuzi wa umma nchini, matumizi ya moduli hiyo katika mnyororo wa ugavi yatachangia kutoa maamuzi kwa haki na wakati na kuwezesha miradi ya serikali

> Inaendelea ukurasa wa 2

PUBLIC PROCUREMENT APPEALS AUTHORITY
Efficient and Fair Appeals Dispensation
PPAA
MAMLAKA YA RUFANI YA ZABUNI ZA UMMA
BULLETIN
UTOAJI RUFAA KWA UFANISI NA HAKI
PPAA
Toleo Na: 09 Aprili - Juni 2026


Toleo Na: 09 Aprili - Juni 2026
BULLETIN
Vijana, makundi maalumu Dodoma, Ruvuma wanolewa kuhusu haki, fursa ununuzi wa umma
Moduli ya Rufaa kuboresha mnyororo wa ugavi

## BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
Florida Mapunda

**Mhariri**
Gloria Tesha
Mwandishi wa TSN

**Wajumbe**
Agnes Sayi
Mohamed Makame
Humphrey Kisanga

**Katibu**
Nelson Kessy

**Mawasiliano:**
**Katibu Mtendaji**
5 Mkandarasi Place,
Ghorofa ya nne, 58
Barabara ya Lusinde,
S.L.P. 1385, 41104 Dodoma
Simu: +255 (0) 743505505,
Baruapepe: barua@ppaa.go.tz
es@ppaa.go.tz
Tovuti: www.ppaa.go.tz

# Moduli ya Rufaa kuboresha mnyororo wa ugavi

*< Inatoka ukurasa wa 1*

kutekelezwa kwa wakati uliokusudiwa," amesema Bw. Sando.

Pamoja na mambo mengine, Bw. Sando amebainisha kuwa matumizi ya Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa katika ununuzi wa umma yatasaidia kuongeza uwazi, kupunguza gharama, kuokoa muda, utunzaji wa nyaraka na hivyo kuongeza ufanisi katika hukumu zinazotolewa kutokana na michakato ya zabuni za umma.

Bw. Sando ameongeza kuwa, PPAA imefanikiwa kushiriki katika utungwaji wa Sera ya Taifa ya Mnyororo wa Ugavi, Sheria ya Ununuzi wa Umma, Kanuni za Ununuzi wa Umma na Kanuni za Rufaa za Ununuzi wa Umma ambapo yote ni michango ya Mamlaka ya Rufani katika mnyororo wa ugavi.

Kadhalika, Mamlaka ya Rufani inatarajia kuboresha kipengele cha makundi maalumu na vijana ambapo inategemea kuboresha gharama au tozo za kesi kwa makundi maalumu pamoja na kuelekeza nguvu kwa vijana na kuhakikisha wanapata fursa ya kudai haki zao katika michakato ya ununuzi wa umma.




*Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando*

Awali, akizindua Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Mnyororo wa Ugavi ya Mwaka 2025, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba (Mb), amezielekeza mamlaka, taasisi na wadau wote wanaosimamia utekelezaji wa sera hiyo kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa kuzingatia misingi ya utawala bora, uwazi na utawala wa sheria.

Waziri Mkuu ametoa maelekezo hayo wakati akizundua sera hiyo kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Dkt. Mwigulu amesema changamoto zinazoikumba sekta ya ununuzi wa umma hazitokani na sera au sheria zilizopo, bali ni uzembe na mitazamo ya baadhi ya watendaji.

Ameongeza kuwa taarifa za ukaguzi kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) pamoja na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) zinaonesha wazi kuwa kasoro nyingi zinasababishwa na utekelezaji dhaifu wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

"Sehemu kubwa ya changamoto hizo zinatokana na hulka, tabia na mitazamo ya watendaji. Hivyo, ni lazima tubadilike ili kufikia malengo ya sera hii," amesisitiza Dkt. Mwigulu.

Aidha, amezitaka wizara, taasisi na mamlaka zote kufanya mapitio ya sera, sheria na kanuni zinazokinzana na sera hiyo ili kuweka mazingira rafiki ya utekelezaji wake.

Naye Waziri wa Fedha, Balozi Khamis Mussa Omar (Mb.) amesema sera hiyo ni mwongozo muhimu utakaosaidia kuimarisha mifumo ya ugavi katika sekta ya umma, kuongeza uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma na kudhibiti vitendo vya rushwa.

Balozi Omar ameongeza kuwa utekelezaji wa sera hiyo utaongeza ajira, kuimarisha mnyororo wa thamani na kuchochea mageuzi makubwa ya kiuchumi kuelekea Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050.



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba (Mb), akizungumza na viongozi wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), alipotembelea banda ya maonesho katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma kabla ya kuzindua rasmi Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Mnyororo wa Ugavi ya Mwaka 2025.*

# Waziri Mkuu aipa Kongole PPAA usimamizi Moduli ya Rufaa

**WAZIRI Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba (Mb.) ameipongeza Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) kwa kuendelea kusimamia matumizi ya moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa kielektroniki.**

Dkt. Mwigulu ametoa pongezi hizo alipotembelea banda la PPAA katika viwanja vya Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma wakati wa Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Mnyororo wa Ugavi ya Mwaka 2025 ambapo Mhe. Mwigulu alizindua sera hiyo kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan.

"Hongereni PPAA kwa kuendelea kusimamia matumizi ya moduli hii, endeleeni kufanya kazi kwa bidii na kuendana na kasi ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan," amesema Dkt. Mwigulu.

Awali, Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando amesema PPAA ni moja kati ya taasisi zinazosimamia ununuzi wa umma nchini, yenye jukumu la kupokea, kusikiliza na kutoa maamuzi ya malalamiko au migogoro dhidi ya taasisi nunuzi ambapo mkataba wa ununuzi au uondoleaji mali tayari umeanza kutekelezwa.

Naye Mkuu wa Sehemu ya Sheria PPAA, Bi. Agnes Sayi amesema kuanza rasmi kwa matumizi ya moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa katika Mfumo wa NeST imesaidia kupunguza gharama, kuokoa muda, kuimarisha utunzaji wa kumbukumbu na hivyo kuongeza ufanisi katika hukumu zinazotolewa na PPAA.

"Mhe. Waziri Mkuu, Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa imesaidia kutoa fursa kwa wazabuni na taasisi nunuzi kuwasilisha malalamiko yao au rufaa kwa wakati na kwa gharama ndogo ikilinganishwa na awali, hivyo kuiwezesha PPAA kutekeleza majukumu yake ya utatuzi wa migogo itokanayo za michakato ya zabuni za umma kwa wakati," amesema Bi. Agnes.



*Sehemu ya viongozi na wadau wa ununuzi wa umma walioshiriki katika uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Mnyororo wa Ugavi ya Mwaka 2025 katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma.*

# Vijana, wafanyabiashara, makundi maalumu waaswa kuchangamkia fursa zabuni za umma

**Serikali ya Mkoa wa Dodoma imewataka vijana, wafanyabiashara, wakandarasi, watoa huduma na wadau wa ununuzi wa umma pamoja na makundi maalumu wa Mkoa wa Dodoma kutumia kikamilifu fursa zinazopatikana katika zabuni za serikali ili kuongeza ushiriki wao katika shughuli za kiuchumi na kuchangia maendeleo ya taifa.**

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhe. Rosemary Senyamule ametoa rai hiyo alipofungua mafunzo ya fursa na haki za wafanyabiashara na makundi maalumu katika michakato ya ununuzi wa umma yaliyoandaliwa na Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) jijini Dodoma, Mhe. Senyamule amesema Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan imeendelea kuimarisha uwazi, uwajibikaji na thamani ya fedha katika sekta ya ununuzi wa umma.

Mhe. Senyamule amesema Serikali inayaoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia imeendelea kuweka mazingira bora ya kuwainua wananchi kiuchumi kupitia mifumo ya ununuzi wa umma inayowezesha wazabuni kushiriki kwa uwazi huku haki zao zikilindwa kwa mujibu wa sheria na kanuni za Ununuzi wa Umma nchini.

Kadhalika, ameipongeza PPAA kwa kuendelea kutoa elimu kwa wafanyabiashara, vijana na makundi maalumu kuhusu fursa zilizopo katika zabuni za umma pamoja na namna ya kushiriki kikamilifu katika michakato hiyo.



*Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhe. Rosemary Senyamule akizungumza na washiriki wa mafunzo (hawapo pichani) juu ya fursa na haki za wafanyabiashara na makundi maalumu katika michakato ya ununuzi wa umma yaliyoandaliwa na Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) jijini Dodoma.*

Mhe. Senyamule amesema bado kuna umuhimu mkubwa wa kuendelea kutoa mafunzo hayo mara kwa mara ili Watanzania wengi zaidi wapate uelewa wa sheria za ununuzi wa umma, haki zao pamoja na namna bora ya kushiriki katika zabuni za serikali.

Kwa upande wake, Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando amesema mafunzo hayo yamelenga kuongeza uelewa wa vijana, wafanyabiashara na makundi maalumu kuhusu haki zao katika michakato ya ununuzi wa umma pamoja na matumizi ya mifumo ya kidijiti katika kushughulikia malalamiko na rufaa.

"Kutokana na maboresho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2023, PPAA imeanza kutumia mfumo wa kielektroniki wa kushughulikia malalamiko na rufaa kupitia Mfumo wa NeST tangu Februari 2025," amesema Bw. Sando.

Bw. Sando amesema matumizi ya Moduli ya kushughulikia Malalamiko na Rufaa katika mfumo wa NeST yameleta manufaa mbalimbali ikiwemo kuokoa muda, kupunguza gharama, kuongeza uwazi na uwajibikaji pamoja na kuweka kumbukumbu sahihi za malalamiko na rufaa zinazowasilishwa na wazabuni.

Bw. Sando ameongeza kuwa, katika mwaka wa fedha 2025/2026, PPAA imefanikiwa kutoa elimu kwa wazabuni 1,296 pamoja na watumishi 705 wa idara za ununuzi na sheria katika maeneo mbalimbali nchini, huku vijana 878 wakipatiwa mafunzo maalumu ya kudai haki zao katika michakato ya ununuzi wa umma kutoka katika mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam, Mwanza na Mbeya.

Kadhalika, Bw. Sando ameongeza kuwa PPAA ina mpango wa kuunganisha Moduli ya kushughulikia Malalamiko na Rufaa na mfumo wa mahakama ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa na kuongeza ufanisi wa utoaji huduma stahiki kwa wananchi kwa wakati kama ilivyosisitizwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050.



*Sehemu ya washiriki waliohudhuria mafunzo yaliyoandaliwa na PPAA kwa ajili ya kuongeza uelewa kwa vijana, wafanyabiashara na makundi maalumu kuhusu haki zao katika michakato ya ununuzi wa umma pamoja na matumizi ya mifumo ya kidijiti katika kushughulikia malalamiko na rufaa.*



*Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando akizungumza na washiriki wa mafunzo (hawapo pichani) kuhusu fursa za haki katika ununuzi wa umma kwa vijana, wafanyabiashara na makundi maalumu.*

# Moduli ya Rufaa kuunganishwa na mfumo wa Mahakama kuboresha upatikanaji wa taarifa

**Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imesema ipo katika mpango wa kuunganisha Moduli ya Kushughulikia Malalamiko na Rufaa iliyopo katika mfumo wa NeST na mfumo wa Mahakama ya Tanzania ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa pale maamuzi ya rufaa yanapopelekwa Mahakama Kuu kwa ajili ya mapitio.**

Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando amesema hatua hiyo inatarajiwa kuanza kutekelezwa mwaka wa fedha 2026/27 ikiwa ni sehemu ya kuimarisha matumizi ya teknolojia na kuongeza ufanisi wa utoaji huduma kwa wananchi sambamba na utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050.

Amesema matumizi ya mfumo wa Mfumo wa Ununuzi wa Umma Kielektroniki (NeST) yameendelea kurahisisha uwasilishaji wa malalamiko na rufaa, kuhifadhi kumbukumbu pamoja na kuongeza uwazi katika kushughulikia mashauri ya zabuni za umma.

“Matumizi ya mfumo huo yamerahisisha utunzaji wa kumbukumbu, kuongeza uwazi katika kushughulikia rufaa na kumwezesha mzabuni kufuatilia hatua iliyofikiwa kwenye shauri lake akiwa popote,” amesema.

Bw. Sando amesema PPAA imeendelea kutoa mafunzo ya matumizi ya mfumo huo katika kanda mbalimbali nchini ikiwemo Kanda ya Ziwa, Kaskazini, Pwani, Nyanda za Juu Kusini pamoja na Kanda ya Kati ili kuongeza uelewa kwa wadau wa ununuzi wa umma.

Amesema katika mwaka wa fedha 2025/2026 mamlaka hiyo imefanikiwa kutoa elimu kwa wazabuni 1,296 na watumishi wa idara za ununuzi pamoja na sheria wapatao 705 kuhusu matumizi ya mfumo wa kushughulikia malalamiko na rufaa.

Aidha, amesema vijana 878 wamefikiwa kupitia mafunzo maalumu yaliyolenga kuwawezesha kufahamu haki zao na kushiriki kikamilifu katika fursa za zabuni zinazotolewa na serikali.



*Sehemu ya washiriki wakifuatilia mafunzo yaliyoandaliwa na PPAA kwa ajili ya kuongeza uelewa kwa vijana, wafanyabiashara na makundi maalumu kuhusu haki zao katika michakato ya ununuzi wa umma pamoja na matumizi ya mifumo ya kidijiti katika kushughulikia malalamiko na rufaa.*

Amesema mafunzo hayo yamekuwa muhimu kutokana na mabadiliko yanayoendelea kufanyika katika sekta ya ununuzi wa umma, jambo linalohitaji wadau kuelewa vizuri taratibu na sheria zilizopo.

Bw. Sando amesema PPAA ni taasisi iliyo chini ya Wizara ya Fedha, ina jukumu la kupokea na kusikiliza malalamiko pamoja na rufaa zinazotokana na michakato ya ununuzi wa umma kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma Namba 10 ya Mwaka 2023.

“Mafunzo haya yanalenga kuwajengea washiriki uwezo wa kutambua fursa zilizopo katika zabuni za serikali, kuelewa haki zao, namna ya kushiriki kwenye zabuni kwa ufanisi pamoja na taratibu za kuwasilisha malalamiko na rufaa,” amesema.

Ameongeza kuwa wataalamu kutoka PPAA, PPRA, Ofisi ya Rais - Maendeleo ya Vijana pamoja na taasisi mbalimbali za kifedha ikiwemo benki wamehusishwa katika mafunzo hayo ili kuwasaidia washiriki kutumia vizuri fursa za ununuzi wa umma kukuza shughuli zao za kiuchumi.

BULLETIN
UTOAJI RUFAA KWA UFANISI NA HAKI
PPAA
Toleo Na: 09 Aprili - Juni 2026

# PPAA yawanoa vijana, makundi Maalumu Ruvuma fursa, haki



*Katibu Tawala Msaidizi Mipango na Uratibu Mkoa wa Ruvuma, Bw. Jumanne Mwankhoo akifungua mafunzo ya siku moja kwa niaba ya Katibu Tawala wa mkoa huo, Bi. Mary Makondo alipomwakilisha katika mafunzo hayo*



*Meneja wa Huduma za Taasisi PPAA, Bw. Paschal Kajuna akitoa hotuba ya ufunguzi wa mafunzo ya siku moja kwa niaba ya Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando alipomwakilisha katika mafunzo hayo.*

**MAMLAKA ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imeendesha mafunzo ya siku moja kwa vijana, wafanyabiashara, wakandarasi, watoa huduma na wadau wa ununuzi wa umma pamoja na makundi maalumu wa Mkoa wa Ruvuma na kuwasihi kutumia kikamilifu fursa zinazopatikana katika zabuni za umma.**

Mafunzo hayo yaliyofanyika katika Halmashuri ya Manispaa ya Songea tarehe 18 Juni 2026 yamelenga kuongeza uelewa wa fursa na haki za vijana, wafanyabiashara na makundi maalumu katika kushiriki mchakato wa ununuzi wa umma.

Akifungua Mafunzo hayo kwa niaba ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma, Bi. Mary Makondo, Katibu Tawala Msaidizi Mipango na Uratibu wa mkoa huo, Bw. Jumanne Mwankhoo amesema Serikali ya Awamu ya Sita imeweka mazingira bora ya kuwainua wananchi kiuchumi kupitia mifumo ya ununuzi wa umma inayowezesha wazabuni kushiriki kwa uwazi huku haki zao zikilindwa kwa mujibu wa sheria na kanuni za ununuzi wa umma nchini.

Bw. Mwankhoo ameipongeza PPAA kwa kuendelea kutoa elimu kwa wafanyabiashara, vijana na makundi maalumu kuhusu fursa zilizopo katika zabuni za umma ikiwa ni njia ya kuwawezesha vijana na makundi maalumu kupata uelewa wa sheria za ununuzi wa umma, haki zao pamoja na namna bora ya kushiriki katika zabuni za serikali.

Kwa upande wake, Meneja wa Huduma za Taasisi wa PPAA, Bw. Paschal Kajuna ambaye alimwakilisha Katibu Mtendaji wa PPAA Bw. James Sando amesema lengo la mafunzo hayo ni kuongeza uelewa wa vijana, wafanyabiashara na makundi maalumu kuhusu haki zao katika michakato ya ununuzi wa umma pamoja na matumizi ya mifumo ya kidijiti katika kushughulikia malalamiko na rufaa.

Bw. Kajuna amesema matumizi ya Moduli ya kushughulikia Malalamiko na Rufaa katika mfumo wa NeST yameleta manufaa ikiwemo kuokoa muda, kupunguza gharama, kuongeza uwazi na uwajibikaji pamoja na kuweka kumbukumbu sahihi za malalamiko na rufaa zinazowasilishwa na wazabuni.

Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, PPAA imefanikiwa kutoa elimu kwa wazabuni 1,717 pamoja na watumishi 705 wa idara za ununuzi na sheria katika maeneo mbalimbali nchini.

Kadhalika, Bw. Kajuna amewataka vijana kuchangamkia fursa za mafunzo zinazotolewa na PPAA ili waweze kunufaika na fursa na haki za vijana, wafanyabiashara na makundi maalumu katika kushiriki mchakato wa ununuzi wa umma.

PPAA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA) imeendesha mafunzo hayo ya siku moja na yamehudhuriwa na washiriki takribani 200 kutoka wilaya za Mkoa wa Ruvuma.

Aidha, mafunzo hayo ni mwendelezo wa mafunzo yaliyotolewa na PPAA kwa Kanda za Pwani, Ziwa, Kaskazini, Nyanda za Juu Kusini na mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza, Mbeya, Iringa, Njombe na Ruvuma.



*Sehemu ya washiriki wa mafunzo ya siku moja kwa vijana, wafanyabiashara, wakandarasi, watoa huduma na wadau wa ununuzi wa umma pamoja na makundi maalumu wa Mkoa wa Ruvuma wakifuatilia mafunzo.*

# PPAA yatupilia mbali Rufaa dhidi ya TBS Kwa kuwasilishwa kinyume na taratibu

**RUFAA iliyowasilishwa dhidi ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS) imetupwa na Mamlaka ya Rufani za Zabuni za Umma (PPAA) kwa kuwasilishwa mbele ya mamlaka hiyo kinyume na taratibu za kisheria.**

Rufaa hiyo iliwasilishwa na kampuni ya **M/S Sunchine Quality Control Technology Service Co. Ltd** mwezi Mei 2026 baada ya kutoridhishwa na uamuzi wa kuondolewa kwenye mchakato wa zabuni ya **utoaji wa huduma za Ukaguzi wa Bidhaa Kabla ya Kusafirishwa (Pre-Shipment Verification of Conformity to Standards – PVoC) kwa bidhaa za kawaida katika Kanda ya China,** inayojumuisha China Bara, Hong Kong, Taiwan, Mongolia na Macau.

Kwa mujibu wa rufaa hiyo, Mrufani alipinga uamuzi wa kuondolewa kwake katika hatua ya uhakiki wa sifa za baada ya tathmini (post-qualification), akidai TBS haikufanya tathmini ipasavyo kuhusu uzoefu wake wa kimataifa, uwezo wa kiufundi, miundombinu ya maabara pamoja na uzingatiaji wa matakwa ya nyaraka za zabuni, licha ya kuwa alikuwa amewasilisha ushahidi wa kutoa kwa mafanikio huduma zinazofanana za ukaguzi wa bidhaa kabla ya kusafirishwa (PVoC) katika nchi mbalimbali.

Mrufani alidai alikuwa na wataalamu wenye uwezo unaohitajika, maabara zilizoidhinishwa pamoja na makubaliano ya ushirikiano katika maeneo ambayo hakuwa na maabara zake binafsi, lakini bado aliondolewa kwa madai ya kutokuwa na umiliki wa maabara hizo. Aidha, alisisitiza kama hatua ya uhakiki wa sifa za mzabuni baada ya tathmini ya zabuni (post-qualification) ingefanyika kwa usahihi, angekidhi vigezo vya kupewa zabuni hiyo. Alidai pia kuwa uamuzi wa kumuondoa ulikiuka masharti ya Sheria ya Ununuzi wa Umma yanayotaka vigezo vya sifa kutumika kwa usawa na kwa uwazi kwa wazabuni wote.


Kwa upande wake, Mlalamikiwa alipinga hoja za rufaa hiyo kwa kueleza kuwa Mrufani alishindwa kukidhi baadhi ya matakwa yaliyobainishwa katika nyaraka za zabuni, ikiwemo kuwasilisha uthibitisho wa leseni za uendeshaji katika maeneo yaliyotajwa, umiliki wa maabara, vyeti vya ithibati (accreditation certificates) kwa Hong Kong na Taiwan pamoja na uthibitisho wa miundombinu ya TEHAMA inayohitajika kwa utekelezaji wa huduma za PVoC. Hivyo, TBS alidai uamuzi wa kumuondoa Mrufani ulikuwa wa haki na ulifanywa kwa kuzingatia masharti ya zabuni na sheria husika.

Kwa kuzingatia hoja za awali zilizowasilishwa kabla ya kuanza kwa usikilizwaji wa shauri, Mlalamikiwa aliwasilisha pingamizi la awali (Preliminary Objection – PO) lenye hoja mbili za kisheria kama ifuatavyo:

1. Kwamba Mamlaka ya Rufani haina mamlaka ya kusikiliza rufaa hiyo kwa sababu ni batili kisheria, ya usumbufu na isiyokuwa na msingi, kutokana na kutokuwepo kwa uamuzi wa Taasisi Nunuzi unaoweza kukatiwa rufaa, kwa kuwa Mrufani hakutumia ipasavyo hatua za awali za malalamiko kwa kuwasilisha malalamiko yake nje ya muda uliowekwa kisheria, kinyume na Sheria ya Ununuzi wa Umma.
2. Kwamba Mamlaka ya Rufani haina mamlaka ya kusikiliza rufaa hiyo kwa sababu iliwasilishwa nje ya muda uliowekwa na Sheria ya Ununuzi wa Umma.

Kuhusu hoja ya kwanza ya pingamizi hilo, TBS aliwasilisha kuwa sheria inaipa Mamlaka ya Rufani mamlaka ya kusikiliza rufaa zinazotokana na uamuzi wa Afisa Masuuli wa taasisi ya ununuzi. Alieleza kuwa, kwa mujibu wa kumbukumbu za rufaa, Mrufani hakuridhishwa na sababu za kuondolewa kwake kama zilivyoelezwa katika notisi ya kusudio la kutoa zabuni ya tarehe 2 Aprili 2026. Hata hivyo, Mrufani aliwasilisha ombi la mapitio ya kiutawala kwa mlalamikiwa tarehe 16 Aprili 2026.

TBS alifafanua kuwa Sheria ya Ununuzi wa Umma inaelekeza namna ya kuhesabu muda, na kwa kuwa Sheria inatumia neno "kutoka", siku ya kuanzia haihesabiwi. Hivyo, kuanzia tarehe 2 Aprili 2026, siku tano za kazi zilimalizika tarehe 14 Aprili 2026. Kwa kuwa maombi ya mapitio ya kiutawala yaliwasilishwa tarehe 16 Aprili 2026, yalikuwa yamechelewa kwa siku mbili. TBS ilisisitiza kuwa kutokana na kucheleweshwa huko, Afisa Masuuli hakuwa na wajibu wa kuyashughulikia maombi hayo, akitegemea kifungu cha 120(4) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma kinachokataza Afisa Masuuli kushughulikia malalamiko yaliyowasilishwa nje ya muda uliowekwa.



Kuhusu hoja ya pili ya pingamizi, TBS iliwasilisha kuwa rufaa iliyoko mbele ya PPAA ilikuwa imepitwa na muda, kwa kuwa iliwasilishwa baada ya kupita siku tano za kazi kama ilivyoelelezwa katika Sheria ya Ununuzi wa Umma. Ilieleza kuwa, kwa kuwa muda wa kuwasilisha maombi ya mapitio ya kiutawala uliisha tarehe 14 Aprili 2026 na maombi yaliyowasilishwa tarehe 16 Aprili 2026 hayakushughulikiwa, Mrufani alipaswa kuwasilisha rufaa mbele ya Mamlaka ya Rufani ndani ya siku tano za kazi kuanzia hapo. Kwa kuhesabu kuanzia tarehe 14 Aprili 2026, muda huo uliisha tarehe 21 Aprili 2026, lakini rufaa iliwasilishwa tarehe 27 Aprili 2026, hivyo ilikuwa imewasilishwa nje ya muda.

Kwa upande wake, Mrufani alijitetea kuwa kifungu cha 121(1) na (2) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma kinamruhusu mzabuni kukata rufaa mbele ya Mamlaka ya Rufani hata pale ambapo Afisa Masuuli wa Taasisi Nunuzi hajatoa uamuzi kuhusu maombi ya mapitio ya kiutawala. Hivyo, hoja ya TBS kuwa Mrufani hakuwa na haki ya kuwasilisha rufaa hiyo haikuwa ya msingi.

Aidha, Mrufani alieleza kuwa chanzo cha shauri kilianza baada ya kupokea barua ya tarehe 20 Machi 2026 iliyomjulisha matokeo ya uhakiki wa sifa baada ya tathmini (post-qualification). Hata hivyo, hakuridhishwa na matokeo hayo, na aliomba ufafanuzi kupitia barua ya tarehe 24 Machi 2026, ambayo ilijibiwa na Mlalamikiwa tarehe 31 Machi 2026. Baadaye, Notisi ya kusudio la kutoa zabuni ya tarehe 2 Aprili 2026 ilitolewa na kupokelewa na Mrufani tarehe 2 Aprili 2026. Hata hivyo, Mrufani aliwasilisha maombi ya mapitio ya kiutawala tarehe 16 Aprili 2026 kupinga matokeo ya uhakiki huo.

Alidai kuwa Notisi ya kusudio la kutoa zabuni ilielekeza kuwa maombi ya mapitio ya kiutawala yawasilishwe ndani ya siku tatu za kazi, jambo ambalo lilikuwa kinyume na kifungu cha 120(4) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma kinachotaka siku tano za kazi. Aidha, Mrufani alikiri kuwa iwapo muda ungehesabiwa kuanzia tarehe 2 Aprili 2026, basi muda wa mwisho ulikuwa tarehe 14 Aprili 2026 na hivyo maombi yaliyowasilishwa tarehe 16 Aprili 2026 yalikuwa nje ya muda. Hata hivyo, aliomba Mamlaka ya Rufani itumie kanuni

*> Inaendelea ukurasa wa 8*

< Inatoka ukurasa wa 7

ya lengo kuu la haki (overriding objective principle au oxygen rule), akisisitiza kuwa haki ya msingi inapaswa kutangulizwa kuliko masharti ya kiufundi ya kiutaratibu.

Kuhusu pingamizi la pili, Mrufani alidai kuwa Mlalamikiwa alimwelekeza kimakosa kwa kuonesha siku tatu badala ya siku tano za kazi kwa ajili ya kuwasilisha maombi ya mapitio ya kiutawala. Alidai taarifa hiyo potofu ilichangia kucheleweshwa kwa uwasilishaji wa maombi ya mapitio ya kiutawala na hatimaye rufaa yenyewe. Hivyo, aliiomba Mamlaka ya Rufani kutumia kanuni ya lengo kuu la haki na kulitupilia mbali pingamizi hilo pamoja na gharama zake ili rufaa isikilizwe kwa kuzingatia hoja zake za msingi.

Katika kuamua pingamizi la awali, Mamlaka ya Rufani ilipitia kumbukumbu za rufaa na kubaini kuwa TBS alitoa Notisi ya Kusudio la Kutoa Zabuni kwa Mrufani tarehe 2 Aprili 2026 kupitia mfumo wa NeST. Mrufani hakuridhishwa na sababu za kuondolewa kwake, hivyo aliwasilisha maombi ya mapitio ya kiutawala tarehe 16 Aprili 2026. Kwa kuhesabu kuanzia tarehe 2 Aprili 2026, muda wa kisheria wa siku tano za kazi uliisha tarehe 14 Aprili 2026.

PPAA ilizingatia hoja ya Mrufani kwamba alipokea Notisi hiyo tarehe 27 Aprili 2026. Hata hivyo, kumbukumbu za shauri zilionesha kuwa tarehe hiyo ndiyo aliyowasilisha rufaa mbele ya Mamlaka ya Rufani. Aidha, Mrufani hakuwasilisha ushahidi wowote kuthibitisha madai yake kuhusu tarehe aliyopokea notisi hiyo.

Zaidi ya hayo, kitendo cha Mrufani kuwasilisha maombi ya mapitio ya kiutawala tarehe 16 Aprili 2026 kilionesha wazi kwamba alikuwa tayari ameifahamu notisi hiyo kabla ya tarehe hiyo. Kwa kuwa notisi ilitolewa kupitia mfumo wa NeST, PPAA iliona kuwa Mrufani hawezi kukana kupokea taarifa hiyo kwa wakati, kwa kuwa mfumo huo hutuma taarifa kwa washiriki wote wa zabuni mara moja. Hivyo, Mamlaka ya Rufani ilikataa madai ya Mrufani kuhusu suala hilo. Kutokana na hali hiyo, PPAA ilibaini kuwa maombi ya mapitio ya kiutawala yaliwasilishwa nje ya muda wa siku tano za kazi uliowekwa na sheria.

Aidha, PPAA ilizingatia hoja ya Mrufani kuhusu matumizi ya kanuni ya lengo kuu la haki (overriding objective principle au oxygen rule). Mamlaka ya Rufani ilieleza kuwa kanuni hiyo haikulenga kuondoa au kupuuza masharti ya lazima ya sheria. Madhumuni yake ni kuhakikisha haki ya msingi inapatikana na kuzuia utegemezi wa kupita kiasi kwenye kasoro za kiutaratibu ambazo hazisababishi madhara au kuathiri mamlaka ya chombo husika. Hata hivyo, kanuni hiyo haiwezi kutumika kurekebisha kutofuata muda wa kisheria au masharti mengine ya lazima yaliyowekwa wazi na sheria.

Kutokana na maamuzi hayo, ambayo yalithibitisha kuwa maombi ya mapitio ya kiutawala yaliwasilishwa nje ya muda uliowekwa na Sheria ya Ununuzi wa Umma, PPAA ilibaini kuwa rufaa ilikuwa na kasoro, hivyo haiwezi kuendelea kusikilizwa.

Kwa msingi huo, Mamlaka ya Rufani ilihitimisha kuwa rufaa hiyo haikuwa imewasilishwa ipasavyo mbele yake na hivyo ikakubaliana na pingamizi la awali lililowasilishwa na TBS. Hivyo, PPAA ilitupilia mbali rufaa hiyo kwa kuwa ilikuwa imewasilishwa mbele ya Mamlaka ya Rufani kinyume na taratibu za kisheria.

## RUFAA DHIDI YA SEKRETARIETI YA MKOA WA PWANI YATUPWA


# Yaagizwa kuanza upya mchakato wa zabuni

**Mamlaka ya Rufani za Zabuni za Umma (PPAA) imetupilia mbali rufaa iliyowasilishwa dhidi ya Sekretarieti ya Mkoa wa Pwani kutokana na muda wa uhalali wa zabuni (tender validity period) kuisha, na kuiagiza taasisi hiyo kuanza upya mchakato wa zabuni kwa kuzingatia matakwa ya sheria husika.**

Uamuzi huo ulitolewa Juni 2026 mbele ya Jaji Mstaafu Mh. Awadh Bawazir katika rufaa iliyowasilishwa na kampuni ya Bei Poa Furniture dhidi ya Sekretarieti ya Mkoa wa Pwani kuhusu zabuni ya Ugavi wa Samani na Vifaa vya Ofisi.

Zabuni ya Mrufani iliondolewa baada ya kubainika kuwa haikukidhi matakwa ya zabuni (non-responsive), kwa kuwa bei aliyowasilisha ilionekana kuwa ya chini kupita kiasi (abnormally low tender). Akiwa hajaridhishwa na uamuzi huo, tarehe 6 Mei 2026 Mrufani aliwasilisha maombi ya mapitio ya kiutawala kwa Mlalamikiwa, tarehe 11 Mei 2026, Mlalamikiwa alitoa uamuzi wa kuyakataa maombi hayo.

Kwa upande wake, Sekretarieti ya Mkoa wa Pwani ilisisitiza kuwa kuondolewa kwa Mrufani kulikuwa halali kwa kuwa aliwasilisha zabuni yenye bei isiyo ya kawaida na alishindwa kutoa maelezo ya kuridhisha kuhusu bei hiyo alipohitajika kufanya hivyo. Mlalamikiwa alieleza kuwa mchakato wa ununuzi ulifanyika kwa kuzingatia sheria, haki na uwazi.



Kabla ya kuanza kwa usikilizwaji wa shauri, Sekretarieti ya Mkoa wa Pwani iliiomba Mamlaka ya Rufani kupokea na kuingiza kwenye kumbukumbu za shauri nyaraka mbalimbali zinazohusu nyongeza ya muda wa uhalali wa zabuni. Mrufani hakupinga ombi hilo, na hivyo Mamlaka ya Rufani iliruhusu nyaraka hizo kupokelewa na kuwa sehemu ya kumbukumbu za shauri.

Kwa upande wake, Mlalamikiwa alieleza kuwa muda wa uhalali wa zabuni husika ulikuwa siku arobaini na tano (45) kuanzia tarehe ya mwisho ya kuwasilisha zabuni, ambayo ilikuwa tarehe 27 Februari 2026. Aliongeza kuwa, kabla ya muda huo wa awali kuisha, Mlalamikiwa alimwomba mzabuni aliyependekezwa kupewa zabuni kuongeza muda wa uhalali wa zabuni kwa siku thelathini (30). Alifafanua kuwa

ombi hilo lilifanywa kupitia barua ya tarehe 26 Machi 2026 na kwamba rejea ya siku arobaini na tano (45) iliyotajwa katika barua hiyo ilikuwa ni kosa la kiuandishi, kwani lengo lilikuwa kuongeza muda kwa siku thelathini (30). Aidha, alieleza kuwa mzabuni aliyependekezwa alikubali ombi hilo kupitia barua ya tarehe 27 Machi 2026.

Aliendelea kueleza kuwa kabla ya muda wa nyongeza ya kwanza kuisha, Mlalamikiwa, kupitia barua ya tarehe 26 Mei 2026, aliomba nyongeza ya pili ya muda wa uhalali wa zabuni kutoka kwa mzabuni aliyependekezwa. Ombi hilo lilikuwa la kuongeza muda kwa siku thelathini (30), kuanzia tarehe 31 Mei 2026 hadi 29 Juni 2026, ambapo ombi hilo pia lilikubaliwa na mzabuni aliyependekezwa tarehe 27 Mei 2026.

Aidha, Mlalamikiwa alieleza kuwa Mrufani hakuombwa kuongeza muda wa uhalali wa zabuni kwa kuwa zabuni yake ilibainika kutokidhi matakwa ya zabuni kutokana na kuwasilisha bei ya chini isiyo ya kawaida na kushindwa kutoa maelezo ya kuridhisha alipohitajika kufanya hivyo. Alisisitiza kuwa kwa mujibu wa Kanuni ya 213 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2024, zabuni ambayo imebainika kutokidhi matakwa lazima ikataliwe na haiwezi baadaye kufanywa ikidhi matakwa kwa kurekebisha au kuondoa kasoro zilizokuwepo. Hivyo, alidai kuwa kuongeza muda wa uhalali wa zabuni ya Mrufani kungekuwa hakuna maana. Kwa msingi huo, alihitimisha kuwa muda wa uhalali wa zabuni uliongezwa kihalali na kwamba zabuni hiyo ilikuwa bado halali hadi tarehe 29 Juni 2026.



Naye Mrufani alidai aliondolewa kwenye mchakato wa zabuni isivyo halali kwa madai ya kutotoa ufafanuzi wa bei aliyowasilisha. Alieleza kuwa hakupokea barua yoyote kutoka kwa Mlalamikiwa iliyomwomba kuongeza muda wa uhalali wa zabuni. Alisisitiza kuwa kwa kuwa alikuwa bado ni mzabuni aliyeshiriki katika mchakato huo wakati ombi la kwanza la kuongeza muda lilipotolewa, naye alipaswa kuombwa kuongeza muda wa uhalali wa zabuni yake.

Alidai sheria inataka maombi ya kuongeza muda wa uhalali wa zabuni yawasilishwe kwa wazabuni wote walioshiriki katika zabuni. Hivyo, kitendo cha Mlalamikiwa kutomwomba kuongeza muda huo kilikuwa kinyume na sheria. Alieleza kuwa kwa kukosekana kwa ombi hilo, muda wa uhalali wa zabuni uliisha mara tu muda wa awali ulipomalizika, na hatua zote zilizochukuliwa na Mlalamikiwa baada ya hapo zilikuwa batili. Aidha, alidai kuwa Mlalamikiwa alifanya ubaguzi kwa kumpa mzabuni mwingine upendeleo usio wa haki. Hivyo, aliiomba Mamlaka ya Rufani iamuru mchakato wa zabuni urudiwe upya kwa kuwa hakukuwa na zabuni halali iliyokuwepo wakati huo.

Katika kuamua hoja za rufaa, Mamlaka ya Rufani ilipitia nyaraka za shauri na kubaini wazabuni walitakiwa kuhakikisha zabuni zao zinabaki halali kwa kipindi kilichobainishwa katika nyaraka za zabuni. Aidha, Taasisi Nunuzi ilikuwa na wajibu wa kuweka muda wa uhalali wa zabuni unaotosha kukamilisha tathmini, kupata idhini ya mapendekezo ya utoaji wa zabuni, kutoa taarifa ya utoaji wa zabuni na kusaini mkataba.

Baada ya kupitia kumbukumbu za rufaa, PPAA ilibaini ufunguzi wa zabuni ulifanyika tarehe 27 Februari 2026 na kwamba muda wa uhalali wa zabuni uliowekwa katika nyaraka za zabuni chini ya vigezo vya tathmini na sifa ulikuwa siku arobaini na tano (45). Kwa kuhesabu kuanzia tarehe 27 Februari 2026, muda huo uliisha tarehe 13 Aprili 2026.

Mamlaka ya Rufani pia ilibaini kuwa Mlalamikiwa aliomba nyongeza ya kwanza ya muda wa uhalali wa zabuni kupitia barua ya tarehe 26 Machi 2026, ambayo ilielekezwa kwa mzabuni aliyependekezwa pekee. Barua hiyo iliomba muda wa uhalali wa zabuni uongezwe kuanzia tarehe 14 Aprili 2026 hadi tarehe 30 Mei 2026, na mzabuni huyo alikubali ombi hilo tarehe 27 Machi 2026.

Kumbukumbu za shauri pia zilionesha kuwa kabla ya muda huo kuisha, Sekretarieti ya Mkoa wa Pwani iliomba nyongeza ya pili ya siku thelathini (30) kupitia barua ya tarehe 26 Mei 2026, ambayo pia ilielekezwa kwa mzabuni aliyependekezwa pekee. Nyongeza hiyo ilihusu kipindi cha kuanzia tarehe 31 Mei 2026 hadi 29 Juni 2026, na mzabuni huyo aliikubali tarehe 27 Mei 2026.

Kutokana na mazingira hayo, PPAA ilibaini maombi yote ya kuongeza muda wa uhalali wa zabuni yaliwasilishwa kwa mzabuni aliyependekezwa pekee. Kitendo hicho kilikuwa kinyume na matakwa ya Kanuni za Ununuzi wa Umma zinazotaka maombi ya kuongeza muda wa uhalali wa zabuni yaelekezwe kwa wazabuni wote walioshiriki katika mchakato husika. Hivyo, nyongeza zilizopatikana kutoka kwa mzabuni mmoja pekee haziwezi kutambulika kuwa halali kisheria.

Aidha, Mamlaka ya Rufani ilibaini kuwa barua ya kwanza ya nyongeza ilihesabu muda wa siku arobaini na tano (45), lakini baada ya uchambuzi wake iligundua kuwa muda ulioongezwa ulikuwa siku arobaini na saba (47), kuanzia tarehe 14 Aprili 2026 hadi 30 Mei 2026. Barua ya pili iliomba nyongeza ya siku thelathini (30) kuanzia tarehe 31 Mei 2026 hadi 29 Juni 2026. Hivyo, kwa mujibu wa nyaraka za Mlalamikiwa mwenyewe, muda wa uhalali wa zabuni uliongezwa kwa jumla ya siku sabini na saba (77).

Mamlaka ya Rufani iliona kuwa kwa kuwa muda wa awali wa uhalali wa zabuni ulikuwa siku arobaini na tano (45), nyongeza yoyote haikupaswa kuzidi kipindi hicho kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma. Hata hivyo, nyongeza ya kwanza ilizidi siku arobaini na tano zilizobainishwa katika nyaraka za zabuni, jambo lililokiuka Kanuni za Ununuzi wa Umma. Kwa hiyo, kuongeza muda wa uhalali wa zabuni kwa jumla ya siku sabini na saba (77) kulikuwa pia ni ukiukwaji wa matakwa ya sheria.

Kutokana na sababu hizo, Mamlaka ya Rufani za Zabuni za Umma (PPAA) ilitupilia mbali rufaa ya Sekretarieti ya Mkoa wa Pwani kutokana na kuisha kwa muda wa uhalali wa zabuni na kuiagiza taasisi hiyo kuanza upya mchakato wa zabuni kwa kuzingatia sheria na kanuni zinazotumika.

# PPAA yashiriki maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma kutoa elimu



*Wananchi wakipata elimu kuhusu ununuzi wa umma, hususan matumizi ya moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko katika mfumo wa NeST, walipotembelea banda ya PPAA kwenye Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyoanza tarehe 16 hadi 23 Juni, 2026 katika Viwanja vya Chinangali Park jijini Dodoma.*




**MAMLAKA ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imeshiriki kutoa elimu kwa wadau wa ununuzi na wananchi kwa ujumla juu ya sekta ya ununzi wa umma katika Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyoanza tarehe 16 hadi 23 Juni, 2026 katika Viwanja vya Chinangali Park jijini Dodoma.**

Maonesho hayo yameratibiwa na Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ikiwa ni sehemu ya jitihada za serikali za kuimarisha uelewa wa wananchi kuhusu fursa na haki katika michakato ya ununuzi wa umma.

Katika maonesho hayo PPAA inatoa elimu kuhusu uamuzi juu ya rufaa zinazotokana na mchakato wa ununuzi wa umma, uamuzi juu ya rufaa zinazotokana na kufungiwa kushiriki katika michakato ya ununuzi wa umma na uamuzi juu ya malalamiko yanayotokana na kushindwa kwa afisa masuuli kutoa uamuzi ndani ya muda uliowekwa.

Maeneo mengine yanayotolewa elimu ni uamuzi juu ya malalamiko baada ya mkataba wa ununuzi kuanza kutekelezwa, uamuzi juu ya maombi ya kuongezewa muda wa kuwasilisha rufaa nje ya muda uliowekwa, uamuzi juu ya maombi ya utekelezaji wa amri ya mamlaka, uamuzi juu ya maombi ya kufuta uamuzi uliotolewa bila kusikiliza upande mwingine (Ex Parte) na uamuzi juu ya maombi ya kurejesha rufaa.

Aidha, wadau mbalimbali wametembelea banda la maonesho la PPAA na kupata fursa ya kufahamu huduma zinazotolewa sambamba na kupata ufafanuzi kuhusu uamuzi juu ya rufaa zinazotokana na mchakato wa ununuzi wa umma nchini.

Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yamefunguliwa rasmi Juni 17, 2026 na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete, (Mb.) ambapo taasisi mbalimbali za umma zimeshiriki maonesho hayo kwa lengo la kuonesha huduma wanazotoa kwa wananchi. Kauli mbiu inasema: Kuchochea Uwajibikaji kwa Huduma Endelevu.




*Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando akizungumza na waandishi wa habari alipotembelea banda la mamlaka hiyo kwenye maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma katika Viwanja vya Chinangali jijini Dodoma.*

# PPAA yajivunia mafanikio ya Moduli ya Malalamiko, Rufaa

**MAMLAKA ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imeendelea kujivunia mafanikio ya matumizi ya Moduli ya Kupokea na Kushughulikia Malalamiko na Rufaa Kielektroniki kupitia Mfumo wa Ununuzi wa Umma wa Tanzania (NeST).**

Mafanikio hayo yamebainishwa na Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando alipotembelea banda la mamlaka hiyo kwenye maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma katika Viwanja vya Chinangali jijini Dodoma.

Bw. Sando amesema kuwa moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa ilianzishwa ili kutatua changamoto mbalimbali zilizokuwa zinajitokeza kwenye utatuzi wa migogoro kwenye michakato ya ununuzi wa umma.

"Changamoto tulizoziondoa kwa wazabuni na taasisi nunuzi ni pamoja na kuokoa muda, gharama, uwazi na uwajibikaji pamoja na kumbukumbu sahihi za malalamiko na rufaa zinazowasilishwa na wazabuni," amesema Bw. Sando.

Bw. Sando amebainisha kuwa ili PPAA iweze kufanya maamuzi kuhusu shauri lililowasilishwa kwa mamlaka hiyo ni lazima kuwa na kumbukumbu sahihi za shauri hilo, hivyo kupitia moduli, PPAA imeweza kupata nyaraka mbalimbali zinazohitajika kwa wakati.

"Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa imeziunganisha taasisi nunuzi na PPAA, faida zote hizi zimeletwa na moduli hii," ameongeza Bw. Sando

"Kwa Mwaka wa fedha 2025/26 hadi sasa malalamiko takribani 157 yamewasilishwa kupitia moduli hiyo kwa taasisi nunuzi, na kati ya malalamiko hayo mashauri 37 yamewasilishwa PPAA na kutolewa uamuzi, hivyo matumizi ya moduli yanaendelea vyema," ameongeza Bw. Sando.

PPAA inampango wa kuunganisha sekta ya utoaji haki katika ununuzi wa umma na mfumo wa utoaji haki wa Mahakama ya Tanzania kwa mwaka wa fedha ujao ili kuongeza uwazi na uwajibikaji zaidi.



*Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando akizungumza na watumishi wa Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora alipotembelea banda la Ofisi ya Rais katika maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma katika Viwanja vya Chinangali jijini Dodoma.*

BULLETIN
UTOAJI RUFAA KWA UFANISI NA HAKI
PPAA
Toleo Na: 09 Aprili - Juni 2026

# HABARIPICHA




*Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhe. Rosemary Senyamule (aliyesimama wa nne kutoka kulia), Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Dodoma, Dkt. Neema Majule (wa pili aliyesimama ktoka kushoto), Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando (wa tatu kutoka kulia), katika picha na baadhi ya washiriki wa mafunzo ya fursa na haki za wafanyabiashara na makundi maalumu katika michakato ya ununuzi wa umma. Mafunzo hayo yaliandaliwa na Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) Mei, 2025 jijini Dodoma.*



*Sehemu ya washiriki wa mafunzo kwa vijana, wafanyabiashara, wakandarasi, watoa huduma, wadau wa ununuzi wa umma na makundi maalumu wa Mkoa wa Ruvuma wakifuatilia mada za mafunzo yaliyoandaliwa na PPAA Juni, 2026 juu ya fursa na haki za vijana, wafanyabiashara na makundi maalumu katika kushiriki mchakato wa ununuzi wa umma.*




*Viongozi wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) wakiongozwa na Katibu Mtendaji, Bw. James Sando (aliyekaa Katikati), Meneja wa Usimamizi wa Rufaa na Sheria, Bi. Florida Mapunda (aliyekaa kulia) na Meneja wa Huduma za Taasisi, Bw. Paschal Kajuna (aliyekaa kushoto) katika picha ya pamoja na watumishi wa Mamlaka ya Rufani baada ya kumaliza kutoa mafunzo juu ya fursa na haki za vijana, wafanyabiashara na makundi maalumu katika kushiriki mchakato wa ununuzi wa umma. Mafunzo hayo yaliandaliwa na PPAA jijini Dodoma mwezi Mei, 2026*